

# **Makosa ya Kiamali katika Kutafsiri Vihisishi: Mifano ya Tafsiri kutoka Kinjeketile (1969) na Amezidi (1995)**

Nahashon A. Nyangeri

## **Ikisiri**

Makosa kuhusiana na tafsiri ya vihisishi aghalabu huwa ni ya kiamali zaidi kuliko kuwa ya kiisimu. Kwa hiyo, mfasiri hana budi kuhakikisha kuwa makosa ya aina hii hayajitokezi kwenye matini lengwa (ML), kwa kuwa hadhira lengwa (HL) huenda ikapata habari za kupotosha. Mfasiri anahitaji maarifa yaliyo zaidi ya uelewa wa kiisimu ili kuibua tafsiri inayofaa. Mara nyingi vihisishi hupewa jukumu la pembeni na wasomi wengi, wakiwamo wafasiri. Inachukuliwa kwamba umuhimu wa kisemantiki, kiamali na wa kimawasiliano kwa jumla wa aina hii ya maneno ni mdogo mno jambo linalosababisha kupuuzwa. Makala inachunguza nafasi ya vihisishi kama aina mojawapo ya maneno yenyе umuhimu mkubwa katika kufanikisha mawasiliano katika tafsiri. Mifano kutoka *Kinjeketile* (Hussein, 1969a) na tafsiri yake ya Kiingereza *Kinjeketile* (Hussein, 1969b) na *Amezidi* (Mohamed, 1995) na tafsiri yake *He is Far Too Much* (wafasiri Weschler na Kimambo, 2012) inaonesha umuhimu wa aina hii ya maneno na changamoto zinazoibuka katika tafsiri. Uchanganuzi linganuzi wa vihisishi katika matini chanzi (MC) na matini lengwa kwa kuzingatia nadharia ya pragmimu au kitendo amali (Mey, 2000; Capone, 2005) unaonesha kwamba mikakati waitumiayo wafasiri si lazima iibue maana kama ilivyo kwenye matini chanzi. Jambo muhimu ni namna ya kuibua athari linganifu kwa misingi ya uamilifu wa matini. Katika hali hii, vihisishi huwa chanzo kikubwa cha makosa ya kiamali. Makala hii inajadili umuhimu huo na jinsi unavyoweza kuzingatiwa katika tafsiri.

## **1.0 Utangulizi**

Vihisishi ndilo kundi la maneno lililopuuzwa kwa kiasi fulani na wataalamu kwa sababu ya mtazamo uliopo kwamba aina hii ya maneno huwa na nafasi ndogo mno katika lugha na kudaiwa kujumuisha faridi zisizo za kiisimu (taz. Quirk na wenzake, 1985; Ameka, 1992). Huweza kufananishwa na ishara na nduni za kisauti kama toni, kiimbo na mkazo. Makosa kuhusiana na tafsiri ya vihisishi aghalabu huwa ni ya kiamali zaidi kuliko kuwa ya kiisimu. Neno amali katika makala hii limetumiwa kwa maana ya utendaji, utekelezaji au pragmatiki. Licha ya vihisishi kuibua changamoto kadhaa za kinadharia na kiufafanuzi, pia vinaweza kuhusishwa na matatizo muhimu ya tafsiri kwa kuwa lugha nyingi hudhihirisha

maumbo sawa au yanayofanana au kuwa na taratibu sawa za uundaji wa maneno lakini kanuni za lugha hizo kuhusiana na matumizi ya vihisishi yakawa tofauti.

Vihisishi huchangia maana ya matini kinyume na mtazamo wa Wharton (2000 na 2003) kuwa havina uzito wowote wa kisemantiki. Wierzbicka (1992) na Wilkins (1992) wanasema, vihisishi vina maudhui fulani ya kisemantiki kwa kuwa vinawasilisha dhana fulani katika mawasiliano. Vihisishi huwasilisha hisia nzito hata pale vinapokuwa havina uhusiano wa kisintaksia na sehemu ya sentensi inayochukuliwa kuwa inabeba wazo kuu. Vilevile, vihisishi vinaweza kuwasilisha toni ya mwandishi au hisia yake au kuuweka ujumbe bayana na kubainisha jinsi unavyofaa kufasiriwa.

Kutokana na ugumu wa kueleza hisia katika lugha andishi, vihisishi hurahisisha jinsi ya kuwasilisha hisia hizo. Hata hivyo, bila umakinifu, vihisishi vinaweza kuonekana kuwa havina maana. Hali hiyo itaishia kusababisha upungufu wa kiamali katika tafsiri. Makala hii hivyo basi inaangazia umuhimu wa vihisishi katika tafsiri. Kadhalika, uchambuzi wa mikakati ambayo lazima itumiwe katika kutafsiri vihisishi ili kuepuka upungufu wa kiamali pia umeelezwa. Makala inatumia mifano kutoka katika tamthilia za *Kinjeketile* (Hussein, 1969a) na tafsiri yake (Hussein, 1969b) na *Amezidi* (Mohamed, 1995) na tafsiri yake *He is Far Too Much* (wafasiri Weschler na Kimambo, 2012),

## **1.1 Vihisishi**

Vihisishi ni kundi muhimu la maneno linaloamua jinsi Hadhira Lengwa (HL) itakavyosoma na kuelewa matini husika. Kushindwa kwa mfasiri kutambua umuhimu wa kisemantiki na kiamali wa vihisishi huishia kuibua tafsiri mbaya. Goffman (1981:100) anadai kuwa vihisishi ni “vitendo vya kimatambiko.” Naye Wharton (2003:40) anadai kuwa hii “si sehemu ya lugha, na huchanganuliwa kwa kuzingatia majukumu ya kijamii na kimawasiliano vinayotekeleza, badala ya maudhui yake ya kiisimu.” Viwe sehemu ya lugha au la, vihisishi ni njia muhimu ya kuwasilisha kila aina ya hisia zetu hivyo kumwelekeza anayezungumziwa kuhusu jinsi ya kuchukulia na kuelewa kinachosemwa. Kutokana na ukweli kwamba tafsiri ni njia ya mawasiliano baina ya wasemaji wa lugha mbili tofauti, vihisishi huwa muhimu kwa mfasiri kwa kuwa huchangia kufikia ulinganifu wa kimawasiliano.

Vihisishi ni vipashio vya kinahau au vya kikaida vinavyowiana na sentensi kisintaksia. Huwa vya kinahau kwa sababu “ni ruwaza za lugha zilizogandishwa kuruhusu tofauti ndogo sana za kimuundo ikiwa italazimu na... mara nyingi kubeba maana ambayo haiwezi kutambuliwa kutokana na vipengele vyake huru” (Baker, 1992: 63). Ni vipashio vya kikaida kwa kuwa vinaweza kuelezwa kama “kauli zilizoratibishwa mapema na kufanywa za kikaida mno kiasi kwamba kutokea kwake hufungamana na hali za kimawasiliano zilizosawazishwa” (Coulmas, 1981:

2-3). Isitoshe, ni aina ya kipekee ya vipashio ambavyo umbo lao huwiana na neno (kama vile lo! sawa! hasa! n.k.) au kishazi (kama vile, Mungu mmoja! Puka chaka! Heri inshalla! n.k.) au sentensi (kama vile ameumaliza wote!) (Cuenca, 2000).

BAKITA (2015) wanaona kuwa vihisishi ni maneno yanayoonesha hisia ya msemaji kama furaha, huzuni, maumivu, hasira na mshangao. Ufafanuzi huu hutegemea zaidi uamilifu wa vihisishi katika lugha. Hata hivyo, hutaja tu maneno pekee bila kuzingatia misemo na vishazi pamoja na baadhi ya ruwaza za sauti na miguno ambazo tulitaja awali kuwa sehemu kubwa ya vihisishi. Katika hali hii, kuna haja ya kuvuka mpaka wa neno ili kueleza maana ya vihisishi. Hii ni ishara ya usemi ambayo hutumiwa kueleza haja fulani, hisia au msukumo wa msemaji kwa anayezungumziwa. Kihisishi hutumiwa kuonesha hisia na hali ya mtu. Kwa sababu hiyo, makala hii inachunguza jinsi hisia zinavyoweza kutafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine.

## **1.2 Upungufu wa Kiamali**

Tafsiri yoyote ile hulenga kutekeleza jukumu fulani kwa wanaolengwa. Katika hali hiyo, pana haja ya kupunguza makosa yoyote yanayoweza kulitatiza lengo hili. Haya yanawezekana tu ikiwa tafsiri itachota kanuni na taratibu kutoka katika Nadharia za Isimu Amali kutekeleza jukumu lake. Katika uchunguzi huu, Nadharia ya Kitendo Amali inatumiwa kuchunguzia jinsi inavyoweza kupunguza makosa ya kiamali katika tafsiri.

Tofauti kati ya kinachotamkwa na kinachomaanishwa ndiyo hudhihirisha upungufu wa kiamali (Thomas, 1983). Hii ina maana kwamba msikilizaji haelewi nia ya msemaji; ingawa anaweza kutambua kosa la kisarufi, lakini asitambue lile la kiamali. Upungufu wa kiamali hautambuliwi kwenye muundo wa nje wa matamko, bali kwa kuchanganua nguvu anazotumia msemaji kujieleza. Haya ndiyo masuala yanayofaa kushughulikiwa katika tafsiri. Ili kufanya hivi, sharti wafasiri wawe na ala zinazohitajika za kujenga uwezo wa kienzoamali kuwawezesha kufanya uchunguzi huo. Kufanikisha hili ni muhimu kutambua aina mbili zilizopo za upungufu wa kiamali – kiisimu-amali na kijamii-amali.

Upungufu wa kiisimu-amali hutokea wakati nguvu ya kiamali ya MC hutofautiana na ile ya ML. Kosa hili hutokana na uhawilishaji wa kiisimu-amali, ambako mikakati ya vitendo-usemi hutumiwa isivyofaa kufasiri kutoka lugha chanzi (LC) hadi lugha lengwa (LL). Kwa mfano, kutumia kauli “Are you serious?” katika Kiswahili kuonya inaweza kuchukuliwa kama swali kubainisha ikiwa msikilizaji ana udhati wa linalorejelewa. Upungufu wa kijamii-amali kwa upande mwingine hutokana na tofauti za kiutamaduni

zinazojenga mionoulimwengu tofauti kuhusu kaida za matumizi ya lugha. Katika makala hii tunajihuisha na aina ya kwanza ya upungufu.

### **1.3 Nadharia ya Kitendo Amali**

Nadharia ya Kitendo Amali iliasisiwa na Gu (1993) na kuendelezwa zaidi na Mey (2001) ili kuziba upungufu wa Nadharia ya Kitendo Usemi (Austin, 1962). Nadharia ya Kitendo Usemi si jumuishi (Fairclough, 1989), haina kipengele cha utendaji na haihusishi muktadha katika ukamilifu wake (Mey, 2001) bali hutegemea zaidi kanuni za ufasaha katika uchunguzi wake. Udhafifu huu, huifanya Nadharia ya Kitendo Usemi isifae kuchunguzia masuala ya tafsiri (taz. Odebunmi, 2006). Katika kuchambua matini, vitendo amali huviweka vitendo usemi kwenye muktadha. Matini hueleweka kikamilifu ikiwa itafafanuliwa ndani ya mazingira ambamo yanahitajika kuwa. Nao wahusika hushiriki kutajirisha usemi au andiko kwa kutumia vidokezo vya muktadha uliopo ili kujaza mapengo (Gu 1993; Odebunmi, 2006). Kwa namna hii hushiriki kujenga maana. Kwa hivyo, kitendo amali huleta pamoja muktadha na washiriki katika uchambuzi wa maana. Kwa hivyo, maana huwa shughuli ya usawazishaji wa maingiliano baina ya wanaowasiliana katika muktadha mahususi. Hii ina maana kwamba kitendo amali ni shughuli ya mapatano ambayo huelekezwa na muktadha (Mey, 2001) kwa kujisilimisha kwenye muktadha na kuyarekebisha mazingira yenewe yawiane na malengo ya mse maji. Kwa hivyo, mse maji hujisilimisha ili kufinyanga usemi wake kwa mujibu wa mazingira anamojikuta wala si kujaribu kuyarekebisha mazingira kupitia kwa usemi wake. Yasiyosemwa huwa muhimu zaidi kuliko yasemwayo. Kwa msingi huu vipengele vya nadharia hii huwa muhimu katika tafsiri ili kuhakikisha maana iliyomo katika MC imehawilishwa hadi ML. Vipengele vya nadharia hii vinavyotumiwa ni:

#### **1.3.1 *Onyesho la Kawaida***

Onyesho la kawaida huhusu “ushirika” unaokuwapo baina ya wahusika ili waweze kuwasiliana katika kiwango sawa. Hili hujengwa na pande zote zinazohusika (taz. Stalnaker, 2002; Enfield, 2008; Jaszczołt, 2008). Ili kufikia hili, sharti vigezo fulani vya maarifa ya kiensaiaklopodia kujitokeza kwa wote kama kirejeleo cha msingi. Hili huwawezesha kuelewa na kufasiri maana. Vigezo hivyo ndivyo hujenga onyesho la kawaida. Onyesho hili hujumuisha masuala zaidi ya muktadha ambao huchukuliwa kuwa jukwaa la pamoja ambamo maingiliano hujitokeza. Masuala haya hujumuisha chukulizi za msingi zinazolifanya onyesho kuwapo.

Onyesho huelekeza utendaji wa washiriki. Yale ambayo onyesho huyamkini yanadhibitiwa na mipaka ya matendo. Matukio ya kawaida yanayoweza kuibuliwa hujenga jukwaa la kijumla kwa utendaji; na ukosefu wake hubana uwezo wa washiriki kutekeleza jambo lolote kijamii. Ingawa utendaji huo

hutegemea uelewa wa washiriki wa onyesho na uwezo wao wa kumudu, onyesho “hutendeka” tu kwa washiriki wote ikiwa limekubaliwa kuwa la jumla kwa wote – yaani, “inayomkiniwa” na wote na kwa wote<sup>1</sup>.

Hali hii inajenga “yanayomkiniwa” ambayo hutuongoza kuelekea fasiri sahihi ya vihisishi, na kwa kweli, ya kile tunachokisema sisi (kwa kuwa hatuiaeleva vilivyo matamko yetu hadi pale kila anayehusika ameyaelewam pamoja nasi). Kwa hivyo, kudakiza kwetu kwenye onyesho la kawaida, kila mara huwa ‘kudakiza kulikokitwa kwenye muktadha mahususi’. Hii ina maana kwamba kihisishi huibuliwa na kumilikiwa na hali mahususi.

### **1.3.2 *Kudakiza Kulikokitwa***

Kitendo usemi husemekana kukiwa ikiwa kinategemea na kujenga hali inayokiwezesha kuibuliwa. Kwa hivyo, kihisishi kilichokitwa hukaribia matukio ya usemi yanayofungamana na shughuli za kiasasi kwenye jamii. Katika shughuli zote kama hizi, jukumu la usemi huwa limeelekezwa; kuna matamko fulani pekee ambayo yanaweza kutarajiwa na kukubalika. Washiriki wanapokubali kinachosemwa kuwa ni tamko lililokitwa kwenye muktadha, wanajenga na kukuza hali zao za kijamii. Msisitizo huwa katika kuchunguza jinsi kitendo fulani kilivyojitokeza kutumiwa kwenye hali na muktadha mahususi na athari zake.

Vitendo usemi hupata nguvu zake kutoka katika hali ambamo vinatamkwa kwa ufaafu. Huu “msaada wa hali” hutokana na kuchukulia kwamba kila hali huwa na kanuni zake. Yaani, kaida na kanuni za jamii huamua njia sahihi ya kudakiza katika hali au muktadha fulani. Kwa hivyo, lazima wasemaji wategemee, na kila mara kupania kujenga, hali ambamo hivyo vitendo amali vinaweza kuibuliwa. Hili huhusisha msemaji kujisilimisha kwa muktadha pamoja na kuusilimisha muktadha kwake. Hii ndiyo sababu vitendo amali vitapotumiwa inavyostahili vinaweza kufaa zaidi kuchanganulia vihisishi.

Isimu-ziada na vipengele vyake kama vile ishara, lafudhi, tambo, mkazo na kiimbo huvifafanua vitendo amali. Maneno kwa upande mwengine yanavifafanua vitendo usemi. Kitendo usemi kinapotamkwa (yaani kinapotamkwa ndani ya muktadha unaofaa) huwa na maana ya muundo mahususi unaochukuliwa na tamko, maingiliano mbalimbali baina ya nduni za muktadha na matini na mazingira ambamo tamko limekitwa pamoja na kanuni za mazingira hayo. Haya ndiyo mambo ambayo kwa pamoja huamua na kuchangia kuamua nafasi ya kihisishi katika jamii zote za ulimwengu. Nduni za muktadha wa kutamka, ambazo husisitiza vipengele vya maana, zitabadilisha maana sisisi ya kihisishi hadi maana ya hali, kuondoa utata na kuweka sahihi hali kwenye tamko, kuweka baadhi ya

---

<sup>1</sup> Neno *mkiniwa* limetumika hapa kwa maana ya “affordances” – yaani uwezo uliomo ndani ya kitendo utokanao na kitu au mazingira hasa kile ambacho kinaweza kuvumbuliwa kwa urahisi.

kanuni za ufasiri zinazohusiana nalo na kujumuisha kundi la vikwazo ambavyo huelekeza jinsi ya kusoma ama kutupilia mbali yale yasiyohusiana nazo au la.

### **1.3.3 Pragmimu**

Pragmimu ni “kitendo usemi kilichokitwa” katika muktadha (Mey, 2001: 94) ambamo kanuni za lugha na za jamii hukutana kupambanua maana huku kikichukuliwa kuwa kitu kilichotambuliwa kijamii kama suala nyeti linaloathiri matarajio kuhusu hali ambamo tamko hufaa kufasiriwa hujitokeza (Capone, 2005). Kitendo usemi kinapokitwa huwa kimepachikwa ndani ya muktadha wa matumizi au wa kanuni unaokiwezesha kufasiriwa kikamilifu. Inahitaji aina tatu za upachikaji: upachikaji wa tamko katika **muktadha wa matumizi** ili kuamua mihimili ya kurejelewa inayokamilisha uashiriaji wa tamko; upachikaji katika **kanuni** ambazo hubadilisha chochote kinachosemwa katika muktadha ili kupata maana inayolengwa; na upachikaji katika **muktadha**, ambao nduni zake huhawilishwa hadi kwa tamko kwa kuondoa utata wa ufasiri na kurutubisha zaidi utajiri wake (wa aina mbalimbali), kwa kuyafanya mahususi zaidi.

Kwa kiasi kikubwa, upachikaji kwenye muktadha ni mchakato wa kifasiri ambao hutajirisha umbo la kauli la tamko na kulipa kile kinacholifanya kupata umahususi zaidi, kama vile kutupilia mbali fasiri nyinginezo mbadala ambazo zinaweza kuthibitishwa kutoka katika aina hiyo ya ukitwaji. Kufasiri tamko kwa kutegemea muktadha wa kijamii wa tamko pamoja na nduni nyinginezo ni jambo la kawaida. Mawazo haya vilevile yanashadidiwa na Capone (2005: 1358) anapodai kuwa, “kaida za kufasiri pragmimu hutokana na mtazamo wa jamii kuhusu lugha.”

Pragmimu ina sehemu mbili: sehemu tendaji na sehemu ya kimatini. Sehemu tendaji huhusisha wanaowasiliana, huku sehemu ya pili ikihusu muktadha wa mawasiliano. Kwa hivyo, pragmimu “hukongamanisha” wahusika na muktadha katika kujenga maana. Sehemu tendaji inaonesha chaguzi zilizopo katika matini kwa washiriki. Hizi ni pamoja na vitendo usemi, vitendo vya kimazungumzo, vitendo vya kisaikolojia, arudhi, vitendo vya kimwili, kusonga kwa mwili, ishara za usoni au fisiognomia, na ishara nyinginezo za mwili. Sehemu ya kimatini ya pragmimu kwa upande mwagine ina “nduni za kimuktadha zinazoathiri mawasiliano” kama vile “ufasiri”, “uhusiano”, “kauli”, “jazanda”, “urejeleaji”, “maarifa ya pamoja yaliyokitwa”, na “kinyago cha kimetapraktiki” (Odebunmi, 2006). Sehemu zote mbili huwa muhimu katika kuelewa pragmimu.

## **2.0 Vihisishi katika Tafsiri**

Uelewa mzuri wa jukumu la vihisishi ni muhimu katika mchakato wa tafsiri. Hufanikisha tafsiri kwa kutambulisha kiini cha mawasiliano (Ameka, 1992). Hata hivyo, isimu haizingatii uchunguzi wa vihisishi kikamilifu kwa kuvichukulia kuwa

ni kundi dogo la maneno yanapolinganishwa na makundi mengine (Cuenca, 2006). Mara nyingi wafasiri hunuia kuhawilisha maana katika MC hadi kwenye ML. Lengo la makala hii ni kuchunguza maana amilifu iliyomo kwenye vihisishi huku msisitizo ukiwa jinsi maana hiyo inavyohamishwa kutoka katika Kiswahili kuelekea Kiingereza kwa kutumia tamthilia za *Kinjeketile* na *Amezidi*.

Smidt (2002) anasema kwamba kihisishi kinaweza kuwa na maana mbalimbali ambazo huweza kuwa kutolewa, kususia kuelewa, kuuliza, kupinga, kukemea, hasira, kukosa subira, tamaa, mshangao, pongezi, kupenda, upinzani na furaha katika viwango vyake mbalimbali. Haya yote hutegemea muktadha pamoja na nia ya msemaji. Kwa kiwango kikubwa vihisishi hutegemea kile msemaji anachotaka kukiwasilisha katika hali ile ambamo vinatumika. Katika hali hii maana yao hudhibitiwa na muktadha kiasi kwamba kihisishi kilekile kinapotamkwa katika miktadha tofauti huwa na maana tofauti (Grice, 1969). Kwa hiyo, huwa ni muhimu kwa mfasiri kuzingatia nadharia za kiamali kutafsiri. Makala hii inatumia dhana ya pragmimu ya Mey (2001) katika uchambuzi wa vihisishi katika tamthilia mbili; *Kinjeketile* na *Amezidi*.

## **2.1 Vihisishi katika *Kinjeketile* na *Amezidi***

Katika sehemu hii tunachunguza aina mbalimbali ya vihisishi vilivyomo katika tamthilia za *Kinjeketile* na *Amezidi* kwa kubainisha mikakati iliyotumiwa kuvitafsiri pamoja na athari za kiamali za tafsiri hizo. Tunaviainisha kisemantiki kwa kuwa maana ndiyo kiini kikuu cha makala hii. Katika uainishaji huo tuna vihisishi vya hisia, amri, na vya utambuzi, ambapo mjadala wa tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

### **2.1.1 Kutafsiri Vihisishi vya Kihisia**

Vihisishi vya kihisia ni vile vinavyowasilisha mchomo wa moyoni, yaani “utambuzi kwa msingi wa hisia” kama vile kero, maudhi, hofu na hasira. Watu huamua kutumia aina hii ya vihisishi kwa sababu wanatambua kitu, tukio, tendo au hali ya mambo inayoibua hisia au mchomo fulani kwa wakati fulani. Hisia, mchomo au mtazamo wenyewe huweza kuibuliwa na vipengele vya kimuktadha vinavyotambulika lakini vilevile huweza kulenga vipengele hivyo. Kwa hivyo, vihisishi vya hisia vinaweza kuchukuliwa kuwa vinabeba taratibu zinazochochea wasikilizaji kuchunguza ni nini kinachoanzisha hisia, mchomo au mtazamo wanaopitia wasemaji na kuueleza unachokilenga.

Damasio (1994) na Goleman (1995) wanataja aina mbalimbali za hisia. Kulingana na Damasio kuna vihisishi vitano: furaha, huzuni, hasira, hofu na kinyaa. Naye Goleman anataja aina nane: hasira, huzuni, hofu, furaha, upendo, mshangao, kinyaa na aibu. Damasio anasema kwamba aina hizi za jumla/kuu za

hisia huwa zina aina nyinginezo za hisia maalum ambazo huwa kama vitanzu vidogo. Kwa hivyo, kusisimka, kuchangamka, kuridhika, kuliwazika, kutetemeka, kutosheka, kupendezwa, kufurahi ni hisia zinazoweza kujumuishwa ndani ya furaha, na huwa mahususi na pambanuzi zaidi. Kwa upande mwingine majonzi, jitimai, sikitiko, simanzi, kibuhuti, sononeko na uchungu zitakuwa ndani ya kihisishi kikuu cha huzuni. Kwa ujumla, mawazo ya wataalamu hawa wawili yanaweza kutufanya tuseme kwamba watu huainisha vikoa vya hisia kwa kutumia dhana za jumla kama zile zinazohusishwa na aina ya hisia wanazopendekeza. Kwa mfano katika *Amezidi*, Ame anapochukizwa na tabia ya mwenzake anayemwamsha bila sababu nzuri anamfokea:

**Ame:** Nini bwana! (uk. 4)

Ame alitarajia kuambiwa jambo la dhati na wala si masuala ya kawaida ambayo labda hufaa zaidi katika soga kwa kuwa ni ya wazi kufahamika kwa kila mtu. Tafsiri iliyotolewa ni:

**Heezfar:** What man! (p. 1)

Kihisishi “bwana” kinachojitokeza hapa kinalipa neno hili maana tofauti na ile ya kikamusi, ambayo imezingatiwa katika tafsiri hii. Hii ni maana ambayo huwasilishwa kuititia ishara zisizo za kiisimu kama vile mkazo, kidatu pamoja na mwonekano wa uso. Kwenye nadharia ya pragmimu, ishara hizi zisizo za kiisimu hujitokeza katika sehemu tendaji. Ikiwa litachukuliwa kuwa “man” (ambalo huwa na maana ama ya “binadamu” au “mwanamume”), hali ya kisaikolojia ya Ame ya kuchukizwa haijajitokeza waziwazi katika tafsiri inayotolewa hapa. Kuna kipengele cha kejeli katika tamko la Ame kinachodokezwa kwa matumizi ya neno “bwana”. Lakini kipengele hicho hupambanuliwa tu kutokana na muktadha wenyewe wala si kutoka katika tamko la Ame. Ni kwa msingi huu inakuwa muhimu kukichunguza kwa mtazamo wa pragmimu. Ame anatarajia zaidi kutoka kwa Zidi badala ya kumwamsha kumwambia masuala madogomadogo jinsi inavyodhihirika kwa kutumia vigezo vya urejeleaji na uhusiano. Tunapozingatia haya yote, tunaona kwamba pana haja ya kuzingatia namna habari hizi zinavyoweza kuwasilishwa katika utamaduni lengwa ili kutekeleza yale yanayotekelizwa katika utamaduni chanzi. Katika hali hii, tafsiri ambayo ingefaa zaidi labda ingekuwa “Mr! What is it?” Hata hivyo, mkakati wa kutumia kauli isiyo kihisishi unasibu hapa pia. Wafasiri wametumia swali badala ya alama ya mshangao ili kufikia uasilia katika tafsiri yao (taz. Cuenca, 2006). Kwa kweli haya huwa ni maswali ya balagha ambayo yamezingatia ukitwaji wa kitamko ili kuelekeza toni yake. Yanapojitokeza kama vihisishi, maswali ya balagha hutumiwa kama changamoto kuwasilishia ujumbe wa kujitolea kwa msemaji kujifunga kwenye maana iliyofichwa ndani ya swali hilo. Lengo huwa kuchochea fikira za msikilizaji kutambua ukawaida anaowasilisha kama anavyofanya Ame. Nyangeri (2014) anasema maswali balagha yanadai jambo linalofahamika

lisilokataliwa. Kwa hivyo huonesha kuchushwa na kuchoshwa kwa msemaji ikiwa yatatumiwa katika muktadha aliyyatumia Ame. Katika hali hii inawezekana kusema kwamba matumizi haya hutambuliwa kutokana na muktadha kwa kuwa yanaweza kutumiwa kumfanya Zidi kukubaliana na msimamo wa Ame.

Mkakati huu wa kutumia muundo usio wa kiingizi unajitokeza pia katika MC umehifadhiwa katika ML kwenye sehemu ifuatayo:

**Ame:** kumekucha? Tokea lini? (uk. 4)

Ingawa hapa inajitokeza kama swali la balagha, nia ya msingi iliyomo kwenye tamko la Ame hubeba pamoja na hayo, vipengele vya hisia za Ame. Maswali kama haya ya balagha huwa na nia ya kumzindua msikilizaji ili awe na mtazamo unaofanana na wa msemaji (taz. Nyangeri, 2014). Swali balagha jinsi lilivyotumika hapa hudhihirisha hisia za Ame za mshangao, dhihaka au kejeli. Kiurejeleaji, Ame anamkejeli Zidi kutokana na kushindwa kwake kutanabahi. Kwa kuwa kauli yake huwa wazi na hulenga tu kuchochea fikira au hisia za Zidi, kifasiri huwa na jukumu la kumdhahiki. Ame anapouliza maswali haya siyo kwamba hajui kuwa kumekucha bali nia yake ni kumzindua Zidi na kumtaka avute tabasuri kuhusu hali yao ya umaskini na utegemezi wao ili afikirie zaidi jinsi wanavyoweza kujikomboa. Hivyo basi, hisia za kujihurumia na kumkejeli mwenzake zinajitokeza hapa. Swali hili lina jukumu la pande zote mbili: Kwanza, kushangazwa kwa Ame, ambaye ni msemaji, kunakochochewa na upumbavu wa Zidi kiasi kwamba hajaukubali ukweli unaojitokeza kuhusu hali yao ya maisha. Ame anaamini kuwa hakujakucha na kushangaa mbinu anazozitumia mwenzake kufikia uamuzi wa kupotosha kuwa kumekucha. Pili ni kumzindua Zidi atambue uhalisi wa maisha yao. Tafsiri iliyotolewa hapa, ambayo haifumbati maana hizi mbili ni:

**Heezfar:** The sun? Since when? (p. 1)

Hata hivyo, mkakati wa tafsiri sisisi uliotumiwa unakosa uasilia kimawasiliano. Kuna chembechembe za ukakasi wa kigeni katika lugha ya Kiingereza. Jua limerejelewa moja kwa moja ilhali maana ashirifu ya kucha inayolengwa hajitokezi; hivyo kupotosha [ujufabiolahassan0@gmail.com](mailto:ujufabiolahassan0@gmail.com)

mbe uliolengwa. Katika MC, Ame anataja msingi wa mshangao wake kabla ya kumfafanulia Zidi kuwa ameshangazwa naye. Kujaribu kudumisha muundo-vihisishi jinsi ulivyo katika lugha ya Kiswahili katika matini ya Kiingereza kunaifanya kazi yenye kosa uasilia. Ni muhimu kutumia mikakati kadha katika sehemu hii ili kuepuka kosa la kiamali linalojitokeza hapa. Jazanda hii katika nadharia ya pragmimu inafaa kuzingatiwa katika kufasiri sehemu hii, badala ya kuzingatia maana rejelevu iliyotolewa. Mkakati kama vile wa kuingiza kirai au msemo, kwa mfano “stop kidding”, ungefaa zaidi hapa ili kuleta maana

iliyolengwa na kauli “tangu lini” kwa kuwa hairejelei wakati. Kwa hivyo, tafsiri faafu ni “Stop kidding! Since when did it dawn?”

Mfano mwingine ambao maana imebadilishwa kutokana na kubadilisha kihisishi ni:

- Zidi:** Aha ... umesema mhogo uliovunda?  
**Ame:** Mhogo uliovunda? Nani kataja mhogo uliovunda au una njaa?  
**Zidi:** Mhogo uliovunda enh!  
**Ame:** Mhogo tokea lini kuvunda?  
**Zidi:** Ah, (*anafanya kukumbuka kitu*) kweli mhogo hauvundi. (uk. 5)

Tafsiri:

- Tumach:** Ah, so you are saying, the cassava that moulded ...?  
**Heezfar:** “The cassava that moulded”? Who mentioned anything about a cassava moulding? Are you hungry or something?  
**Tumach:** enh, the cassava that moulded!  
**Heezfar:** Since when does cassava mould?  
**Tumach:** Ah! (*pretends to have suddenly remembered something*) of course. (p. 2)

Katika sehemu hii kuna viingizi kadhaa. Aha! katika Kiswahili hutumika kuashiria utambuzi wa ghafla. Msemaji anaelewa kwa ghafla kitu, tukio, jambo au hali ambayo awali hakuielewa (Wamitila, 2003: 269; BAKITA, 2015: 14). Kihisishi kinachoshabihiana na hiki katika Kiingereza huwa na maana sawa na hii. Hata hivyo, tafsiri iliyotolewa hapa ni “Ah!” Hiki ni kihisishi kinachotumiwa kuonyesha mshangao, furaha, pongezi, huruma, kuchanganyikiwa au msemaji kutokukubaliana na jambo (OUP, 2010). Kwa hiyo, mfasiri anaamua kutumia kihisishi chenye maana tofauti. Kwa kuwa Zidi analenga kuwasilisha furaha aliyonayo kuwa ameelewa ujumbe wa Ame kuwa anarejelea ‘mhogo uliovunda’, basi kihisishi sahihi kingekuwa aha!

Huruma ni mojawapo ya hisia ambayo wanaowasiliana hawana budi kuiwasilisha kila mara. Mojawapo ya matamko wanayoyatumia wasemaji ni “Maskini” kuwasilisha hisia hii. Neno hili limetumiwa na Hussein (1969a) pale Bibi I anapomhurumia Chausiku ambaye ameenda shambani mwa bwana Kinoo kulima badala ya mumewe. Anamhurumia Chausiku kwa kuwa anafahamu kuwa askari wanaweza kumdhulumu Chausiku. Bibi I anasema:

- Bibi I:** Maskini Chausiku! Na huyu Mnyapala kwenda kumpelekea yule askali-ndiyo nini? (uk. 11).

Hisia za huruma alizo nazo Bibi I zinajitokeza hapa. Hisia hizi hufaa kuhawilishwa katika ML. Tafsiri iliyotolewa ni:

- First Woman:** Chausiku – poor girl! (*she shakes her head.*) And this Mnyapala, of all the things to do! Why, did he have to procure Chausiku for the Askari, a young and green maiden like that? (p. 11).

Kwa kuhisi kwamba tafsiri iliyopo ya neno kwa neno haiwasilishi hisia za Bibi I, mfasiri anaongeza maelezo ya ishara ya anayoitumia msemaji ya kutikisa kichwa. Hii inachochewa na ukweli kwamba huenda ikawa na maana ya mtu asiyekuwa na bahati inavyojitokeza katika kauli “**poor stiff**”.

Mkakati huu wa kuongeza maelezo yasiyokuwamo katika MC kwa lengo la kubainisha hisia inayojitokeza umetumiwa pia katika mazungumzo ya ufunguzi ya Bibi I na Bibi II. Wanapotaniana kuhusu jinsi waume wao hukosa hamu kutokana na kazi nyingi wanayoifanya, Bibi I anasema:

**Bibi I:** Na ye ye hakutamani (*wanacheke*) (Hussein 1969a: 11)

Lakini tafsiri iliyotolewa imeongezewa kihisishi cha kuwasilisha hisia za furaha ambazo zimewasilishwa kupitia maelezo yaliyomo.

**First Woman:** Ah, so she doesn't turn towards you! (*She laughs mischievously*) (Hussein 1969b: 11)

Kiingizi “**Ah!**” kilichoongezwa kimechochewa na muktadha wa mawasiliano uliomo katika MC. Lengo hasa ni kubainisha hisia ya furaha inayotawala katika sehemu hii.

Vipo viingizi vya kimuktadha ambavyo hujitokeza kama mateteo katika tamthilia ya *Kinjeketile*. Huwa na jukumu la kupinga au kukubaliana na kinachowasilishwa. Kila mara Kitunda anapowahamasisha watu wanaitikia kukubali kwa kusema “Maji! Maji! Maji!” kihisishi hiki cha kimuktadha kimehawilishwa jinsi kilivyo hadi ML. Hakuna sababu maalumu ya mfasiri kufanya hivi. Katika baadhi ya sehemu fasiri ya “water” imetumika huku kwingine neno maji likitumiwa. Katika mfano ufuatao, fasiri iliyotolewa imehamisha moja kwa moja yaliyomo.

**Wote:**  
Maji!  
Maji!  
Maji! Kinjeketile!  
Maji! Kinjeketile! Maji! (Hussein 1969a: 16)

**Crowd:**  
Maji!  
Maji!  
Maji! Kinjeketile!  
Maji! Kinjeketile! Maji! (Hussein 1969b: 18)

Uhamishaji huu hauwezi kuwasilisha ujumbe uliomo kwenye MC hadi ML. Hisia ya umoja wa watu ambaa umetokana na nguvu ya maji ya Kinjeketile inahitaji kushirikishwa katika fasiri hii. Hiyo ndiyo hisia ambayo imekitwa katika kauli ya maji. Kwa hivyo ni muhimu kutumia neno la Kingereza “water”.

Jukumu la vihisishi katika Kiswahili na jinsi vinavyoshughulikiwa katika tafsiri huweza kuibua tatizo lenye uhusiano na masuala ya kiisimu-amali na

umahususi wa kitamaduni. Masuala haya hutatiza mawasiliano baina ya tamaduni tofauti. Ni kweli kwamba, “tafsiri ya kihisishi inaweza kuwa ya asili moja na ya LC” (Aijmer, 2004) na kupunguza matatizo ya tafsiri. Kihisishi “ah!” cha Kiingereza huwiana kifonolojia na “aha!” katika Kiswahili. Hata hivyo, maneno yanayoshabihiana yanaweza kuhusiana kwa kiwango cha kifonolojia na kimofolojia pekee wala si kisemantiki au kipragmatiki. Katika Kiingereza hutumiwa “kuwakilisha kelele ambayo watu hufanya katika mazungumzo kuelezea faraja au mshangao” (Collins-Cobuild, 1995: 1140), lakini katika Kiswahili kinatumika kuonesha kukubali au kuitikia, furaha, uchungu au kukataa (Wamitila, 2003; TATAKI, 2013). Kwa sababu hiyo, kiini cha tatizo la kutafsiri vihisishi linaweza kuelezwaa kwa kuzingatia umuhimu wake wa kiamali, ambao huenda ukamtatiza mfasiri.

### **2.1.2 Kutafsiri Vihisishi vya Amri**

Vihisishi vya amri ndivyo huwa vya wazi zaidi na hutumiwa kuwasilisha ujumbe wa kuelekeza, kuagiza au kuamuru. Anayevitumia vihisishi vya aina hii huwa anasema kile anachokitaka anayemlenga akifanye. Kwa mifano, msemaji anapotamka “us!” au “buu!” au “shhhh!” anamaanisha “ninataka unyamaze”. Watu hutumia vihisishi hivi wanapotaka mwenzao kutekeleza au kutotekeleza jambo fulani. Hivyo huelekezwa pande zote mbili: huelekezwa kwa matendo au hali ambayo msemaji anawasilisha kuwa inafaa, na mtu anayetarajiwaa na msemaji kutenda au kuibua hali anayoitaka. Kwa hivyo, vihisishi vya amri vinaweza kuchukuliwa kubeba taratibu za kuhamasisha wasikilizaji kutafuta kile ambacho msemaji anatarajia mtu akifanye au kutofanya pamoja na kutaja mtu huyo ni nani.

Mojawapo ya viingizi tata na telezi kutafsiri ni hodi. Hiki ni kiingizi kinachoonesha haja ya anayebisha kuruhusiwa kuingia ndani. Katika *Amezidi* kiingizi hiki “hodii” (uk. 23) kimetafsiriwa kuwa “knock-kock” (uk. 22). Huu ni mifano halisi wa kiingizi, ambacho Wilkins (1992) anakiita leksimu isiyo kamilifu, ambacho hutoa tu fununu vuguvugu kuhusu kile msemaji anataka kukiwasilisha. Tafsiri inayotolewa ni maelezo ya kinachopaswa kufanyika wakati mtu anataka kupewa kibali kuingia ndani ya nyumba. Hii inadhihirisha upungufu mkubwa wa kiamali kwani nia aliyonayo mhusika Mari anapobisha mlangoni hajitokezi kwa vyovoyote vile. Changamoto hapa ni kwamba katika utamaduni wa ML, dhana ya kuomba kuingia hutekelezwa kwa njia tofauti na ya MC. Katika hali hiyo, kunakosekana tamko la moja kwa moja la kutumia kuwasilisha nia hii.

Utata huu pia unajitokeza katika *Kinjeketile* (Hussein 1969a:8) pale Mnyapala anapokitumia kihisishi hiki kuomba kufunguliwa na Kitunda. Anasema, “Hodi! Hodi! Fungua. Hodi! Fungua.” Tafsiri iliyotolewa imehamisha kihisishi hiki jinsi kilivyo pasi kutoa hata maelezo yoyote ili kumwezesha msomaji wa ML kuelewa matumizi yake. Katika ML Mnyapala anasema “Hodi! Hodi! Open the

door!” (Hussein, 1969b: 9). Neno hodi katika LL ni geni hivi kwamba msomaji hutatizika kufahamu matumizi yake. Matumizi ya vihisishi kama vile “Haloo!” “Hey!” au “anybody in!” hufaa zaidi (taz. pia Loogman, 1965). Katika muktadha wa utamaduni wa LL, “Hallo!” na “Hey” hutumiwa kuvuta nadhari ya anayelengwa. Kwa sababu hii, pragmimu inayolengwa ni kuvuta nadhari ya mlengwa hivyo kutumia vihisishi hivi hufaa zaidi.

Inavyoonekana, mara nyingi ni vigumu kupata visawe sahihi vya kimuktadha vya vihisishi au hata ufanuzi wake. Aina hii ya vihisishi hutumiwa katika sentensi kuonesha uchangamfu wa mtu na haja yake ya kukutana na msikilizaji. Inaweza kuchukuliwa kuwa ni kuonesha haja ya kutaka kuingia. Lakini, inaweza kutumika kueleza hisia ambapo msemaji huonesha furaha yake kwamba atapata fursa kukutana na mtu anayemtarajia. Tafsiri iliyotolewa hapa inabadilisha kile kinachowasilishwa katika MC ambacho ni “haja” ya kuingia. Lakini, kwenye tafsiri haja hii inakuwa maelezo ya nia ya kuingia nyumbani kuitia kwa kugonga mlango. Huku ni kukiuka wazo la Wharton (2003) kwamba, vihisishi *huonesha* badala ya *kusema*. Hata hivyo, ni lazima ieleteke kwamba pia inawezekana kwa baadhi ya vihisishi kuwa na maana ambayo haiwezi kuwasilishwa kwa kutumia maneno kwa sababu watu wanakosa dhana imara ya kuiwakilisha maana hiyo. Hivyo, maana yenyewe inaweza kusimbiliwa kwa kutumia virai au sentensi.

Hasira huweza kuandamana na matumizi ya vihisishi vya amri. Msemaji huweza kumfokea mhusika aliyemkera huku akiambatanisha usemi wake na masharti anayoyataka kutekelezwa. Bi. Kitunda katika *Kinjeketile* (Hussein, 1969a: 9) anawakemea Mnyapala na Kitunda kwa kukosa ujasiri.

**Bi Kitunda:** Tokeni! Tokeni, wanawake wakubwa nyi! Vijuvi vilivili vinawatisheni – nyinyi nyote. Mmetawaliwa miili mpaka mioyo. Eti nyinyi wanaume kweli. Kweli Wamatumbi, hata kidogo. Wanawake tu nyinyi! Nnalimishwa – ndiyo.

Hii ni sehemu ambayo imejaa vihisishi vya hisia na vya amri. Ifuatayo ndiyo tafsiri iliyotolewa (Hussein, 1969b: 10):

**Bi Kitunda:** Get out! Get out of here, you women, you! Two little men were enough to scare the whole lot of you. You have been enslaved body and spirit. Do you still regard yourselves as men? Do you call yourselves Wamatumbi? Oh no, not at all. You are mere women, you! You are forced to dig – yes.

Kwenye tafsiri hii, hasira ya Bi Kitunda imemchochea kuwaamuru kutoka. Hata hivyo katika tafsiri yenyewe, kiwango cha hisia za Bi. Kitunda kimepunguzwa. Hili linatokana na kubadilisha njeo iliyotumika. Kwa kutumiwa wakati uliopita, amri iliyomo katika MC inabadilishwa na kujitokeza kama kejeli. Isitoshe kutafsiri neno vijuvi kuwa “little men” kunaondoa makali yaliyomo katika kauli hii. Vijuvi

lililotumika hubeba uzito wa kuwashurutisha wahusika kuchukua hatua kuitetea jamii yao. Kwa msingi huu matumizi ya neno “**imp**” yangemfaa zaidi.

Huwa kawaida katika mawasiliano mtu anapozungumza kuwataka wengine wawe watulivu kuyasikia anayotaka kuyasema. Mzungumzaji anaweza kuwasihii au kuwashurutisha wamsikilize. Kitunda katika *Kinjeketile* (Hussein, 1969a: 13) anawasihi wengine kuwa watulivu hata kuungwa mkono na Mtu I. Sehemu hii haitatizi katika tafsiri iliyotolewa (Hussein, 1969b: 14).

### **2.1.3 Kutafsiri Vihisishi vya Utambuzi**

Vihisishi vya utambuzi huwasilisha ujumbe unaoegemea zaidi kwenye ung’amuzi na ufahamu wa hali ya habari, yaani kile ambacho mtu anajua, anaishia kujua, alichokijua n.k. Kwa mfano, Sadakta! Pongezi! Shukrani! Aina hii ya viingizi huingiliana na vile vya hisia kwa sababu huwa na kipengele cha hisia ndani yake. Tazama mifano ifuatayo kutoka *Amezidi* (Mohamed, 1995):

- Zidi:** Aaaa – si usiri tu! Mtu husema leo nitanunua na jua liangukapo anajikuta hajanunua na ifikapo kesho ameshasahau ... hivyo hivyo mpaka ulimwengu uishe!
- Ame:** Sasa tutafute kijiti basi!
- Zidi:** Ee, nawe umezidi tena! Uvivu tu! Kuamka niamke mimi, mhogo nikachimbe mimi na kibenza ... (uk. 10)

Sehemu hii imetafsiriwa ifuatavyo:

- Tumach:** Ah, isn’t it just dilly-dallying, though? You say, “I’ll buy it today”, but when the sun waves goodbye you find yourself not having bought nothing. And by the time tomorrow comes around, you’ve forgotten. Just like that ... till the end of time.
- Heezfar:** Let’s look for a twig, then!
- Tumach:** eeh, there you go again. You’re really too much! Plain laziness! I’m the one who digs for cassava with a splinter... (uk. 10).

Mkakati wa tafsiri sisisi ambao umetumiwa hapa huingiza vionjo vya kigeni kama ilivyo kwenye dondoor lifuatalo pia:

- Ame:** Hamna! Lo! Tutakufa basi ... au unatania? (uk. 6)
- Heezfar:** There isn’t? Lo! We’ll die, then ... or is this a joke? (uk. 4)

Muundo wa kiingizi ‘hamna!’ katika MC kama mshangao umebadilishwa kuwa swali kwenye ML. Mkakati huu tumeushughulikia hapo awali. Kimsingi “hamna!” hutumika kuonesha mshangao. Kwa mujibu wa TUKI (2004:108) hamna huwa na maana ya “kutokuwamo kitu ndani ya.” Katika hali hii matokeo huwa tofauti na yanayotarajiwa pale tafsiri inayotolewa ni ‘there isn’t’. ‘Isn’t’ linapotumika kama kihisishi huibua dhana kwamba kauli inayohusishwa nacho ni ya kejeli au kinaya (Oxford Advanced Learner’s Dictionary of Current English, 2010). Kutumia “no” badala ya “there isn’t” ni bora zaidi kwa kuwa mojawapo ya sifa za viingizi ni

iktisadi au ufupi. Kwa hiyo, kutumia maneno machache hufaa zaidi. Vinginevyo mkakati wa kutoa maelezo ya ishara za uso na mikono kudhihirisha hali kupitia maelezo ya uigizaji ingefaa zaidi kama vile kusema ‘*akionesha kushangaa usoni na kukodoaa macho.*’

Tafsiri imedumisha kiingizi “lo!” ambapo katika Kiswahili hutumika kuonesha wasiwasi, furaha, hofu au mshtuko kulingana na mazingira (Wamitila, 2003; BAKITA, 2015). Viingizi vyta Kiingereza ambavyo hutumika kuwasilishia hisia hizi ni pamoja na “ahh!” na “ehe!” (Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English, 2010). Mantiki ya kudumisha kiingizi hiki cha “kigeni” katika ML si wazi. Hatuwezi kusema kwamba hisia inayowasilishwa hapa haiwasilishiki katika lugha ya Kiingereza. Hervey (1998) anasema kuwa, jamii zote zina uwezo wa kueleza wazo, na hata hisia ambayo huwasilishwa na utamaduni mwagine. Kuteua kiingizi “ahh!” kungefaa zaidi katika tafsiri.

Udondoshaji ni mkakati mwagine unaotumika katika kutafsiri vihisishi vyta utambuzi. Huu ni mkakati wa kutohamisha kihisishi kilicho katika MC hadi ML. Kwa mfano:

**Ame:** Ah ... unakusudia hiyo BMW na Mercedes zetu hapo nje? (uk. 17)

Katika hali ambamo vihisishi vimegotanishwa na kauli nyingine, kama hapo juu, ni rahisi kuona kwamba hisia, mchomo au mtazamo umeelekezewa kauli hiyo. Wharton (2003) anakiri kuwa ujumbe uliomo ndani ya vihisishi unatofautiana kulingana na hali mahususi. Katika dondoo hili, furaha ya Ame inadhihirika kwa sababu anamiliki magari ya gharama kubwa. Hata hivyo, haya yameachwa kwenye tafsiri iliyotolewa kama inavyoonekana hapa chini:

**Heezfar:** Might you be referring to that MBW and Mercedes of ours, out there?  
(p. 20)

Katika aina hii ya tafsiri, kihisishi *ah* ambacho kimedondoshwa, kinaweza kujitokeza kwa kutegemea ishara za kiziada zilizo nje ya lugha kama vile toni na mkazo, vipengele ambavyo hutumika katika lugha ya mazungumzo. Katika hali hii, iwapo mkakati wa kuacha unatumiwa basi sharti utumike kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa unapunguza athari ya kipragmatiki ya matini. Ikiwa mfasiri anataka kudumisha yaliyomo katika kihisishi, kuna haja ya kuongeza au kufafanua zaidi pale ambapo hakuna kihisishi cha kuwasilisha ujumbe unaolengwa kikamilifu katika ML, kwa mfano:

**Zidi:** Aa, haya...bado ...bado kabisa! Hakujacha kamwe (*anatikisa kichwa*) (uk. 4)

Hapa Zidi anaonyesha kukerwa na upumbavu wa Ame. Katika kuwasilisha hisia hii kwenye tafsiri, mkakati wa kuongeza umetumika ili kufafanua matendo ya mhusika ambayo yataweka wazi habari hizi.

**Tumach:** (sarcastically) Alright, then ... not yet ... not at all (p. 1)

Njia nyingine ambayo mkakati wa kuongeza umetumika ni kwa kutumia tanbihi. Haya ni maelezo yanayotoa taarifa za usuli kwa HL. Kwa mfano:

**Ame:** Unajua tena kufaliwa leo, kesho kuna Mungu ... ah, ati kazi ... kazi, kazi ... sasa kazi ndiyo maana yake sio? (uk. 7)

**Heezfar:** And you know, for today, we'll be tided ... and for tomorrow, there is God. Ah, so work ... work ... work now, that is work, no? (p. 5)

Katika tafsiri iliyotolewa tumeambiwa katika tanbihi kwamba sehemu hii ni changamano na haieleweki kwa urahisi kwani si wazi. Wakati mwingine mbinu hii hutumiwa na mfasiri kukwepa jukumu la kumwasilishia msomaji habari za kimsingi ambazo huipa matini utajiri mkubwa katika uibushi wa maana. Hapo awali tulisema kwamba kitu chochote kinachosemwa katika utamaduni mmoja kinaweza pia kusemwa katika utamaduni mwingine. Pengine katika kiwango cha neno, hili haliwezekani lakini katika kiwango cha maana kwa hakika hili linawezekana. Maana haimo kwenye maneno bali kwenye muktadha. Maneno hutumiwa tu kuandamana na muktadha ili kumchochea msomaji kuibua maana kwa kutajirisha usemi wa msemaji. Katika tanbihi hii, hata huo utata wanaodai wafasiri kuwapo, wameutaja tu bila kuufafanua. Huku ni kukwepa jukumu na kujificha nyuma ya pazia la mkakati wa kuongeza kuititia tanbihi. Mikakati ya kutumia kutafsiri imepangwa na Cuenca (2000) kwa utaratibu wa 'ni upi uanziwe na upi uwe wa mwisho'. Katika mpangilio huo, mkakati wa kuongeza taarifa na kufafanua ndio wa mwisho kabisa. Inaajabisha kuona kwamba mkakati huu umetumiwa mno katika tafsiri ya tamthilia ya *Amezidi*, ilhali unafaa kutumika pale hiyo mingine inapokuwa imeshindwa kabisa. Swali tunalojiuliza ni je, ni vigumu mno kutafsiri kazi za Kiswahili kwenda Kiingereza kiasi kinachofanya mkakati wa kufafanua utumike zaidi? Hebu tazama tafsiri walivotoa wafasiri wa *Amezidi* hapa chini:

**Heezfar:** You know what? We live each day at a time, Let us worry of today for God knows our tomorrow. Ah! Talking of work ... work ... work ... so this is the meaning of it all, work, or what is your opinion? (p. 5)

Kutokana na tafsiri hii tunaweza kutoa maoni yetu kwamba maana imo katika muktadha na wala si katika maneno yanayotumiwa, hususani tunapotafsiri vihisishi. Maneno huwa ala tu anayoitumia msemaji kumkaribisha msikilizaji katika kuumba maana. Kwa namna nyingine, maneno huwa kiandamizi katika safari ya kuisaka maana iliyomo katika muktadha. Katika hali hiyo basi ni muhimu mfasiri aelewé ni maneno (ala) gani yanayofaa katika mazingira gani kama ilivyo dhahiri kuwa kila sherehe huwa na mtindo wake wa mavazi.

Kuepuka kuzingatia muktadha pamoja na pragmimu katika tafsiri huishia kupotosha maana inayowasilishwa. Katika *Kinjeketile* (Hussein 1969a: 2) Bi. Kitunda anasema:

- Bi Kitanda:**
- Akuna nyoka,
  - Akuna nyoka,
  - Tazama,
  - Yuko nyoka?
  - Akuna nyoka.

Lengo hasa la Bi Kitunda ni kumshawishi Chausiku kuamini kwamba nyoka hakuwapo. Ili kufasiri hili jinsi inavyostahili, ni muhimu kuzingatia onesho la kawaida wanalolijenga Bi Kitunda na Chausiku ili kukita kudakiza kwao inavyostahili. Haya ndiyo huwawezesha kushirikiana kujenga maana kuwa hakuwapo nyoka. Onesho lililoko hapa hudhihirisha kwamba, Chausiku ama anafanya mzaha kuhusu kuwapo kwa nyoka au pengine amechanganyikiwa. Pale wanapoelewana kuwa kauli ya Bi Kitunda inafaa kufasiriwa hivyo basi wamejenga onesho la pamoja watakalolitumia kuifasiri kauli yake na kudakiza inavyolengwa. Tafsiri iliyotolewa ni ya kisemantiki tu isiyozingatia masuala haya ya kiamali ambayo huzingatia muktadha:

- Bi Kitunda:
- There is no snake,
  - There is no snake,
  - Look, is there a snake?
  - Of course not,
  - There is no snake. (p. 3)

Hata hivyo, kihisishi cha tazama kimetafsiriwa kisemantiki hivyo kupoteza kiwango cha uhisisvu katika ML. Katika kufikia maana hii iliyomo, tafsiri imetaja kuwa, kwa kweli nyoka hayupo. Ni kwa sababu hii, mkabala wa kiamali unapendelewa katika makala hii. Matumizi ya “**come on!**” kutafsiri kihisishi hiki yanafaa zaidi.

Pale ambapo hakuna kauli andamizi kwa kiingizi, Wharton (2003) anasema kwamba vihisishi huibua hisia kuelekea kwa kitu, jambo au tukio linalosababisha mwitikio mahususi. Hisia hizo hazifafanuliwi kwa maelezo bali huwasilishwa jinsi zinavyojiteza moja kwa moja. Yaani haziwezi ‘kuwakilishwa’ na vipashio vingine ambavyo sizo hizo hisia. Anatoa maoni kwamba vihisishi husimba maana ambayo inaweza kufananishwa na maelekezo ya kutia wasikilizaji moyo kupata ala za kimuktadha ambazo zinawasaidia kuelewa kikamilifu zaidi kile wasemaji wanachokipitisha, yaani nia arifu.

### 3.0 Mapendekezo

Makala hii imeshughulikia tatizo la kutafsiri vihisishi. Hii ni sehemu ya lugha ya hisia ambayo ni sehemu pana mno kiasi kwamba haiwezekani kuchunguzwa

kikamilifu katika makala moja pekee. Hii ni kwa sababu vitambulishi nya aina hii ya lugha ni vingi mno. Kuna vitambulishi nya kisauti, kiishara na kimaumbile ambavyo tunapendekeza kuwa vitafitiwe. Isitoshe, utafiti umejifunga kwenye tamthilia mbili tu. Kuna haja ya kuhusisha kazi nyingine za kifasihi na za tanzu mbalimbali na vipindi mbalimbali nya utunzi. Vilevile, kushughulikia matumizi ya sajili mbalimbali ili kuichunguza kwa kina nadharia yenyewe jinsi inavyochangia kuibua namna ya kufasiri maana. Hii itasaidia kufikia uamuzi na hitimisho mwafaka zaidi.

#### **4.0 Hitimisho**

Katika makala hii tunaweza kusema kuwa vihisishi ni vipengele muhimu katika tafsiri kama aina ya mawasiliano. Vihisishi visipotafsiriwa ipasavyo, tafsiri zinazoibuliwa hupungukiwa kiamali. Kutokana na mjadala wetu tamthilia za *Amezidi* na *Kinjeketile* ni za kihisia zaidi kuliko kuwa za mawasiliano ya kawaida. Tofauti hii inajitokeza kupitia matumizi mengi ya nduni zinazohusishwa na lugha ya kihisia ambayo hujumuisha vihisishi. Vilevile, uchunguzi umeonesha kuwa mikakati mbalimbali imetumiwa katika kutafsiri vihisishi. Hii ni pamoja na kukiacha kihisishi, kufafanua zaidi, kubadilisha kihisishi, na kutumia kihisishi chenye maana tofauti na ya MC. Maoni yetu kuhusu mikakati hii ni kwamba kutafsiri kihisishi katika ML kwa kutumia kihisishi kilicho na maana sawa na ya kile cha MC huwasilisha maana kwa mkazo sawa na ule uliomo kwenye MC. Maana ya vihisishi vingi huhusiana na muktadha. Katika hali hii uelewa wa vihisishi hutegemea kile msemajji anachotaka kukiwasilisha katika muktadha huo. Hii ina maana kwamba kihisishi kilekile kinaweza kuwa na maana tofauti kutegemea muktadha wa matumizi. Vilevile, maana hiyo inaweza kuwa ya muda huohuo tu wa kutamkwa na hata ikawa maana ngeni wala si ile ya kikaida au ya kila siku. Hii ni maana funge ambayo hueleweka tu katika muda mahususi tu.

Makala hii imeonesha kwamba kutafsiri vihisishi ni suala la kisemantiki na la kiamali. Sharti mfasiri atambue maana za kisemantiki na kiamali pamoja na muktadha wa matumizi, kisha achunguze umbo ambalo litaeleza maana hiyo na kuibua athari hiyohiyo kwa hadhira inayolengwa. Ni kwa sababu hii, mkabala wa kitendo pragmatiki hufaa katika upataji wa maana iliyomo katika kihisishi cha MC na kuihawilisha maana hiyo katika ML.

#### **Marejeleo**

- Aijmer, K. (2004). Interjections in a Contrastive Perspective, in W. Edda (Ed.), *Emotion in Dialogic Interaction: Advances in the Complex*. Philadelphia: John Benjamins, pp. 99-120.
- Ameka, F. (1992). Interjections: The Universal yet Neglected Part of Speech, *Journal of Pragmatics*, 18(2/3):101-118.

- Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation*. London: Routledge.
- BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.
- Beaugrande, R.D . (1988). *Critical Discourse: A Survey of Contemporary Literary Theorists*. New Jersey: Ablex.
- Capone, A. (2005). Pragmemes: A Study with Reference to English and Italian, *Journal of Pragmatics*, 37: 1355 - 1371.
- Catford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation: An Essay in Applied Linguistics*. London: Oxford University Press.
- Collins, C. (1995). *Collins Cobuild Advanced Dictionary*. Birmingham: Collins Cobuild.
- Coulmas, F. (1981). Introduction: Conversational Routine, in F. Coulmas (ed.), *Conversational Routine. Explorations in Standardized Communication Situations and Prepatterned Speech*. The Hague: Mouton, pp. 1 - 17.
- Cuenca, M. J. (2000). Defining the Indefinable? Interjections, *Syntax*, 3: 29 - 44.
- Cuenca, M. J. (2006). Interjections and Pragmatics Errors in Dubbing, *Meta*, 5(1): 20-35.
- Damasio, A. (1994). *Descartes' Error: Emotion, Reason and the Human Brain*. New York: Avon.
- Enfield, N.J. (2008). Commonground as Resource for Social Affiliation, in I. Kecske, & J. Mey. (eds.), *Intention, Common ground and the Egocentric Speaker-Hearer*. New York: Mouton de Gruyter, pp. 223-254.
- Goffman, E. (1981). *Forms of Talk*. Oxford: Blackwell.
- Goleman, D. (1995). *Emotional Intelligence*. New York: Bantam Books.
- Grice, H.P. (1969). Meaning, *The Philosophical Review*, 66: 377 - 388.
- Gu, Y. (1993). The Impasse of Perlocution, *Journal of Pragmatics*, 20: 405–432.
- Hervey, S. G. (1998). Speech Acts and Illocutionary Function in Translation Methodology, in L. Hickey (ed.), *The Pragmatics of Translation*. Johannesburg: Multilingual Matters. pp. 10 - 24.
- Hussein, E. M. (1969a). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, E. M. (1969b). *Kinjeketile* (E. M. Hussein Trans.) Nairobi: Oxford University Press.
- Jaszczolt, K. (2008). Psychological Explanations in Gricean Pragmatics and Frege's Legacy, in I. Kecske, & J. Mey (eds.), *Intention, Common ground and the Egocentric Speaker – Hearer*. New York: Mouton de Gruyter. pp. 9 - 44.
- Kurzon, D. (1998). The Speech Act of Incitement: Perlocutionary Acts, *Journal of Pragmatics*, 571 – 596.

- Loogman, A. (1965). *Swahili Grammar and Syntax*. Pittsburgh: Duquesne University Press.
- Mey, J. (2001). *Pragmatics*. Oxford: Blackwell.
- Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohamed, S.A. (2012). *He's Far Too Much*. (S. Weschler, & N. Kimambo, Trans.) Nairobi: Longhorn.
- Nida, E., & Taber, C. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E.J. Brill.
- Nyangeri, N. A. (2014). Vitendo Usemi na Ulinganifu wa Maana katika Tafsiri: Mifano kutoka Tafsiri za Kazi Mbili Teule za Barbara Kimenye. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Odebunmi, A. (2006). A Pragmatic Reading of Yerima's Proverbs in 'Yemoja Attahiru' and 'Dry Leaves on Ukan Trees', *Intercultural Pragmatics*, 3(2): 153-170.
- Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English*. (2010). Nairobi: Oxford University Press.
- Quirk, R., Greenbaum, S., Leech, G., & Svartvik, J. (1985). *A Comprehensive Grammar of the English Language*. London: Longman.
- Scott-Tennent, C., Davies, M., & Torras, F. (2000). Translation Strategies and Translation Solutions: Design of a Teaching Prototype and Empirical Study of its Results, in A. Beeby, D. Ensinger, & M. Presas (eds.), *Investigating Translation*. Amsterdam: Benjamins, pp. 107 – 116.
- Searle J.R. (1969). *Speech Acts: An Essay in the Philosophy of Language*. London: Cambridge University Press.
- Smidt, K. (2002). Ideolectic Characterisation, *A Doll's House. Scandinavica*, 41(2): 191-206.
- Stalnaker, R. (2002). Common ground, *Linguistics and Philosophy*, 25: 701-721.
- Thomas, J. (1983). Cross-cultural Pragmatic failure, *Applied Linguistics*, 4(2): 91-112.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Wharton, T. (2000). Interjections, Evolution and the 'Showing/Saying' Continuum, *The Evolution of Language Conference*. 18. Paris: Université de Paris.
- \_\_\_\_\_. (2003). Interjections, Language, and the 'Showing/Saying' Continuum, *Pragmatics and Cognition*, 11(1): 39 - 91.
- Wierzbicka, A. (1992). The Semantics of Interjection, *Journal of Pragmatics*, 18: 159-192.
- Wilkins, D. P. (1992). Interjections as Deictics, *Journal of Pragmatics*, 18: 119-158.